**HOTUBA YA MHE. MKUU WA WILAYA YA MPWAPWA KWA AJILI YA UZINDUZI WA UNYWESHAJI WA DAWA KINGA/TIBA ZA MINYOO YA TUMBO NA KICHOCHO MASHULENI KATIKA WILAYA YA MPWAPWA TAREHE 02 MAY 2019.**

**Ndugu Viongozi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama,**

**Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Mpwapwa,**

**Viongozi wa Dini,**

**Wakuu wa Idara,**

**Viongozi wa Kisiasa,**

**Ndg. Wananchi,**

**Mabibi na Mabwana.**

**Ndugu wanachi,** Awali ya yote yatupasa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kutuwezesha kukutana leo mahali hapa. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kamati ya maandalizi kwa kunikaribisha kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huu muhimu wa unyweshaji wa dawa Kinga/Tiba za magonjwa ya minyoo ya tumbo na Kichocho kwa watoto wetu wa shule za msingi. Aidha niwapongeze wananchi wote wanaozunguka shule zetu za Mtejeta na Chazungwa mlioacha shughuli zenu na kukusanyika nasi kwa ajili ya uzinduzi wa shughuli hii muhimu.

**Ndugu wananchi**, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo: IMA WORLD, wamelenga kutoa dawa Kinga/Tiba kwa ajili ya minyoo ya tumbo na kichocho katika Mikoa mbali mbali Tanzania ukiwemo Mkoa wetu wa Dodoma. Serikali imeamua kutoa dawa hizi kwa sababu magonjwa haya hayapewi kipaumbele kama magonjwa mengine (mfano Malaria, HIV na Kifua Kikuu) licha ya kwamba yana madhara makubwa katika jamii na kwa wananchi wetu.

**Ndugu wananchi,** magonjwa ambayo hayapewi kipaumbele ni pamoja na Ukoma, ugonjwa utokanao na kuumwa na mbwa au mnyama mwenye kichaa (rabies), ugonjwa wa Tauni, Matende na Mabusha au Ngirimaji, Trakoma, Kichocho, Minyoo ya tumbo, Usubi, Homa ya dengi, Homa ya Malale na Homa ya Ini.

**Ndugu wananchi,** magonjwa haya ambayo hayapewi kipaumbele yana madhara makubwa kwa waathirika na kwa Taifa kwa ujumla. Baadhi ya madhara ya magonjwa haya ni maumivu ya muda mrefu na wakati mwingine ulemavu mkubwa, huchangia umaskini na hudumaza uchumi wa taifa, hudhoofisha ukuaji na maendeleo ya mtoto kimwili na kiakili katika umri mdogo, na vifo kwa waathirika. Bila shaka baadhi yenu mmekutana au kuwaona wagonjwa wenye matende wanavyotaabika na kuumia na pia wale wanaougua kansa ya kibofu cha mkojo au Ini. Hakika madhara haya ni makubwa.

**Ndugu wananchi**, magonjwa haya yanaambukizwa kwa njia mbali mbali. Hapa nitagusia magonjwa ya Kichocho na minyoo ya tumbo ambayo ndiyo yanatusumbua sana katika maeneo yetu. Kichocho husababishwa na minyoo inayoitwa "Schistosoma". Minyoo hii huenezwa na konokono anayetoa vimelea kwenye maji yaliyotuama kama kwenye majaruba ya mpunga au mabwawa. Ugonjwa huu wa kichocho husababisha damu kuonekana kwenye mkojo na choo, na mgonjwa asipotibiwa mapema kikamilifu, ugonjwa husababisha saratani ya tumbo, kibofu cha mkojo na Ini.

Ugonjwa wa minyoo ya tumbo husababishwa na minyoo ya aina tatu: minyoo mviringo, minyoo mjeledi na minyoo ya safura. Minyoo hii huenezwa kwa kula uchafu kama vile matunda yasiyosafi, chakula kilichopoa na ambacho hakikufunikwa vizuri na maji ambayo hayakuchemshwa. Vile vile minyoo hii huenezwa kwa kutembea bila viatu mahali palipo na minyoo hiyo. Minyoo hii husababisha Mtu kuwa dhaifu na kuishiwa damu, tumbo kuuma, utumbo kujifunga au kutoboka na kifafa.

**Ndugu wananchi**, kila mara tunasisitiziwa kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Magonjwa haya niliyoyataja yana njia mbali mbali za kujikinga nayo. Baadhi ya njia hizo ni kuzingatia usafi wa mwili kwa ujumla wake, kuzingatia usafi wa mazingira kwa ujumla, kutokuoga/kutokuogelea/kutokutembea kwenye maji yasiyo safi na yaliyotuama kama vile mabwawa na mifereji, na kutumia dawa za kutibu na kudhibiti magonjwa haya.

**Ndugu wananchi**, Wilaya yetu imepata fursa kushiriki katika zoezi hili la kutoa dawa za Kinga/Tiba kwa watoto walioko katika shule za msingi Mwezi huu Aprili 2019. Mwezi wa nane tutashiriki kutoa dawa kwa watoto walioko nyumbani wenye umri wa miaka mitano hadi 14. Zoezi hili linafanyika katika shule zote za Msingi 126. Katika zoezi hili tumelenga kuwafikia watoto 73,000. Nasisitiza kuwa ni vizuri tutumie fursa hii ya kupata dawa Kinga/Tiba.

**Ndugu wananchi**, kutokana na umuhimu wa zoezi hili, ninawaombeni sana mtoe ushirikiano wa kutosha kwa kuhakikisha watoto wetu walengwa wa zoezi hili, walioko katika shule za msingi wenye umri wa miaka mitano hadi miaka 14 wanakunywa dawa ili tuweze kufikia lengo letu la kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na afya bora

**Ndugu wananchi,** napenda kuwahakikishia nyinyi nyote kuwa dawa hizi zinazotolewa katika vituo vyetu ni salama na zimethibitishwa na shirika la Afya Duniani (WHO), na zinatolewa na wataalamu wenye uzoefu mkubwa waliobobea katika fani hii kwa muda mrefu. Na asiwepo mtu yeyote kupotosha juu ya zoezi hili. Dawa hizi zinatibu endapo unavyo vimelea vya magonjwa husika na hutukinga na ugonjwa endapo huna vimelea vya ugonjwa.

Nanyi wanafunzi mkiwa na minyoo au vimelea vya magonjwa kama kichocho afya zenu zitazoofika na uwezo wa kufikiri unapungua na hata hamtaweza kujifunza vizuri na hivyo kushindwa kufikia malengo ya ufauli kishule, Kiwilaya, Kimkoa hadi Kitaifa.

Kutokana na madhara ya magonjwa haya, Serikali yetu ya awamu ya tano, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo IMA WORLD na wengine wanaogharimia mpango huu imeamua kugawa dawa hizi bure bila gharama yoyote kwa wananchi wake ili kuboresha Afya zao.

Nisisite kuwa usafi wa mazingira ni nguzo kuu katika kuimarisha Afya zetu. Nawaasa wananchi wote kuhakikisha kuwa mazingira yetu majumbani na sehemu za kazi yanakuwa safi kila siku. Nanyi wanafunzi mnatakiwa kuwa wasafi, mazingira ya shule zenu siku zote yawe safi. Tumieni vyoo vyenu vizuri ili muepukane na magonjwa ya minyoo na kuhara. Walimu shirikianeni katika zoezi hili la kugawa dawa kwa wanafunzi wenu.

Ndugu wananchi, nihitimishe kwa kuwashukuru tena kwa kuhudhuria katika shughuli hii ya uzinduzi wa unyweshaji wa dawa Kinga/Tiba za magonjwa ya minyoo ya tumbo na Kichocho mashuleni katika Wilaya yetu.

Baada ya kusema hayo naomba kutangaza kuwa shughuli hii ya uzinduzi wa unyweshaji wa dawa Kinga/Tiba za magonjwa ya minyoo ya tumbo na Kichocho kwa watoto wa shule za msingi katika Wilaya yetu nimeizindua rasmi.

**Asante kwa kunisikiliza, Mungu awabariki.**